

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA TATU

02 SEPTEMBER, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA TATU – TAREHE 02 SEPTEMBER, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2021*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2021*].

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**30. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN
KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- (a) Je, ni lini Serikali itapeleka Watumishi na vitendea kazi vya kutosha katika Zahanati mpya 24 zilizojengwa ndani ya Halmashauri ya Mji wa Geita;
- (b) Je, ni lini Serikali itadhibiti upotevu wa mapato katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya.

**31. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE
SAMIZI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Hayati Dkt. John Magufuli, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu ya kujenga Kituo cha Afya Kata ya Murungu katika Wilaya ya Kibondo ili kusogeza huduma na kupunguza msongamano wa Wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo.

32. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa jengo la Manispaa ya Tabora ambao umesimama kwa muda mrefu huku shughuli za Manispaa zikiendelea kufanyika kwenye majengo ya zamani yaliyochakaa.

33. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza kazi ya ujenzi wa mradi wa Mto Msimbazi ambao umetajwa katika Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

34. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaendeleza kimasomo Watoto wa kike waliokatisha masomo kwa kupata ujauzito.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

35. MHESHIMIWA CAPT. ABBAS ALI MWINYI (FUONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

- (a) Je, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ina Taasisi ngapi na zipi kati ya hizo zina uwezo wa kujiendesha zenyewe;
- (b) Je, zipi kati ya Taasisi hizo zinapeleka gawio Serikalini;
- (c) Je, gawio ni takwa la Kisheria.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

36. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kuwatambua na kulinda maslahi ya Vijana waliojajiri katika Sanaa ya Burudani kama *Video Vixen* na *Video King*.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

37. MHESHIMIWA JOSEPH KIZITO MHAGAMA (MADABA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

- Je, ni lini Serikali itachukua hatua kudhibiti watu wanaodanganya kupeleka Ng'ombe katika Mnada wa Mtyangimbole kisha kuwatorosha na kuwaingiza katika maeneo mbalimbali ya Madaba, Namtumbo na Songea ilihali Madaba haina uwezo wa kuhimili wingi wa mifugo hiyo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

38. MHESHIMIWA OMAR ALI OMAR (WETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itatoa ajira kwa Jeshi la Polisi hasa ikizingatiwa kuwa haijatoa ajira tangu Mwaka 2015.

WIZARA YA KILIMO:

39. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua Kituo cha Utafiti na Uzalishaji Mbegu cha SKU – SULUTI cha Shirika la Kilimo Uyole kilichopo

- Wilayani Namtumbo ambacho kwa sasa hakifanyi kazi na majengo yake yameharibika.

V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2021*].

**DODOMA
02 SEPTEMBER, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**